Wito kwa Rais Samia

Kuhusu Tarehe
29 Mwezi wa Kumi
Kila Mwaka Kutengwa Kuwa Siku ya Kitaifa ya Kumbukizi ya Matukio na Wahanga Wa

Tarehe 29 Octoba 2025



Kaulimbiu:

"Kumbukizi, Ukweli, Haki, Uwajibikaji na Uponyaji— Kamwe Yasijirudie Tena."



1.0 UTANGULIZI

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), ukiwa ni mtandao wa kitaifa unaoratibu na kuunganisha mashirika ya utetezi wa haki za binadamu nchini, ulitoa pendekezo mwaka jana na kulirejesha tena mwezi Februari 2026 la kuitambua rasmi tarehe 29 Oktoba ya kila mwaka kuwa Siku ya Kitaifa ya Kumbukizi ya Matukio na Wahanga wa matukio yaliyotokea kuanzia Oktoba 29, 2025 wakati wa uchaguzi na maandamano. ***"Heri wapatanishi, maana hao wataitwa wana wa Mungu." (Mathayo 5:9)***

Leo, ikiwa zimebaki siku chache kufikisha mwaka mmoja tangu kutokea kwa matukio hayo ya kusikitisha, tunapenda kurejea tena ushauri huu na kuwakumbusha viongozi wakuu wa nchi, wakiwemo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na taasisi nyingine za kitaifa zenye mamlaka ya maamuzi, kutafakari kwa uzito umuhimu wa kutenga tarehe 29 Oktoba kuwa Siku ya Kitaifa ya Kumbukizi ya Matukio na Wahanga wa Oktoba 2025.

Kuna umuhimu mkubwa kwa taifa kuwakumbuka na kuwaenzi Watanzania waliopoteza maisha katika matukio yaliyotokea wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa tarehe 29 Oktoba 2025, kutambua maumivu ya familia, majeruhi na wananchi wengine walioathirika, waliopoteza mali, na kujifunza kutokana na historia hiyo. THRDC inaamini kuwa lengo kuu la kumbukizi hii si kuwakumbuka wahanga pekee, bali kuhakikisha kwamba matukio yanayosababisha upotevu wa maisha, ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu na matumizi yasiyo halali ya nguvu hayajirudii tena nchini Tanzania. ***"Hakuna mustakabali usiohitaji msamaha, lakini hakuna msamaha wa kweli usiohitaji ukweli." Desmond Tutu***

Katika kujenga uponyaji na maridhiano ya kitaifa, tunakumbushwa kuponya waliovunjika moyo na kupatanisha wanaovutana. ***'Waumini ni ndugu; basi patanisheni kati ya ndugu zenu' (Qur'an 49:10),*** na kwamba 'Huponya waliovunjika moyo, na kuyafunga majeraha yao' (Zaburi 147:3). Mafundisho haya yanatutaka kutafuta ukweli, kutenda haki, kuponya majeraha ya wahanga na kujenga taifa lenye mshikamano ili matukio kama haya yasijirudie tena.

Pendekezo la THRDC linazingatia pia mapendekezo ya Tume ya Rais ya Kuchunguza Matukio ya Uvunjifu wa Amani Wakati na Baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025,



iliyoongozwa na Jaji Mkuu Mstaafu Mohamed Chande Othman. Katika uwasilishaji wa ripoti yake tarehe 23 Aprili 2026, Tume hiyo ilipendekeza Serikali kutenga siku maalumu ya maombolezo ya kitaifa kwa ajili ya kuwakumbuka waliopoteza maisha katika matukio hayo. THRDC inasisitiza kuwa, kwa kuwa tarehe 29 Oktoba 2026 inatimiza mwaka mmoja tangu matukio haya kutokea, ni vyema kama taifa kuitumia siku hiyo kutafakari na kujadiliana namna tunavyoweza kuponya majeraha hayo, pamoja na kuweka mikakati ya pamoja ya kuzuia matukio haya yasijirudie na kufanyia kazi visababishi vyote vilivyotajwa na wananchi pamoja na Tume ya Chande. Kwa unyenyekevu mkubwa, tunamshauri Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kuona umuhimu wa kufanyia kazi suala hili kwa manufaa ya mshikamano na utulivu wa taifa.

Katika kujenga taifa lenye maridhiano ya kweli, ni muhimu kuhakikisha kuwa kumbukizi hii haigeuki kuwa chanzo cha chuki, uhasama au kulipiza kisasi. Badala yake, iwe fursa ya kutafakari kwa pamoja, kutafuta ukweli, kuimarisha haki na kujenga mshikamano wa kitaifa. Kama Qur'an inavyotukumbusha: ***"Enyi mlioamini! Kuweni wasimamizi imara kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, mkitoa ushahidi kwa uadilifu. Wala kuchukiana na watu kusikufanyeni msifanye uadilifu. Fanyeni uadilifu, kwani huo ndio ulio karibu zaidi na uchamungu. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyatenda." Suratul Maaidah (5:8).***

"Mwenye kufanya uombezi mzuri, ana fungu lake katika hayo; na mwenye kufanya uombezi mbaya, naye ana sehemu yake katika hayo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu." An-Nisa 4:85

Lengo kuu la siku hii ni kutambua na kuenzi historia ya matukio ya Oktoba 2025 kwa kuwaheshimu wahanga na walioathirika, kuhifadhi kumbukumbu sahihi za kihistoria, kuhamasisha ukweli, haki na uwajibikaji, kukuza uponyaji, mshikamano na maridhiano, pamoja na kufuatilia maboresho ya kisheria, kisera na kitaasisi ili kuzuia matukio kama hayo yasijirudie. Kuwakumbuka wahanga si tendo la huruma pekee, bali ni wajibu wa kibinadamu na kiroho unaotukumbusha kuwa sote ni ndugu katika maumivu na matumaini.

“THRDC inaamini Kumbukizi ya kweli si kukaa katika maumivu ya jana, bali kuyabadilisha kuwa hekima ya kesho, haki kwa walioumia, na dhamira ya pamoja kwamba kamwe yasijirudie tena."



2.0 SABABU KUANZISHA SIKU YA KITAIFA YA KUMBUKIZI

a) Kuzuia Kujirudia kwa Mauaji naUkiukwaji Mkubwa wa Haki- "Yasijirudie Tena"
Sababu ya msingi zaidi ni kuhakikisha taifa linajifunza kutokana na matukio ya Oktoba 2025 na kuchukua hatua madhubuti kuzuia kujirudia kwa vifo, majeruhi na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu. Kumbukizi isibaki katika maombolezo pekee, bali iwe siku ya kutathmini hatua za kuboresha sheria, sera, taasisi na uwajibikaji. Falsafa ya "Yasijirudie Tena (Never Again) iwe ahadi ya pamoja ya kuheshimu uhai na utu wa kila Mtanzania.

b) Kuwakumbuka na Kuwaenzi Wahanga na Familia zao
Kila maisha yaliyopotea yana thamani. Kumbukizi itatambua historia, mchango na utu wa wahanga na kutoa fursa ya taifa kuonesha pole na mshikamano kwa familia, majeruhi na jamii zilizoathirika. Iwe jumuishi bila ubaguzi wa kisiasa, kidini, kijinsia au kijamii na ihamasishe upatikanaji wa huduma na msaada unaostahili.

c) Kuhifadhi Historia ya Taifa na Kumbukumbu kwa Vizazi Vijavyo
Historia ya taifa inapaswa kuhifadhi mafanikio na pia matukio magumu ili vizazi vijavyo viweze kujifunza. THRDC inapendekeza ukusanyaji wa nyaraka, taarifa zilizothibitishwa, tafiti na ushuhuda wa hiari kwa kuzingatia ridhaa, faragha na usalama. Kumbukumbu hizo zitumike kufundisha kuhusu uhai, Katiba, utawala wa sheria na utatuzi wa migogoro kwa amani.

d) Kukuza Ukweli, Haki na Uwajibikaji
Kumbukizi yenye maana inahitaji kujengwa sambamba na uchunguzi wa kuaminika, upatikanaji wa haki kwa wahanga na uwajibikaji pale makosa yatakapothibitishwa. Itumike kutathmini hatua za uchunguzi, mapendekezo ya tume, msaada na fidia stahiki, pamoja na mifumo inayozuia kutokuwajibishwa. Maridhiano hayawezi kuwa mbadala wa ukweli, haki na uwajibikaji.

e) Kujenga Uponyaji, Umoja na Maridhiano ya Kitaifa
Matukio yanayosababisha vifo na vurugu yanaweza kuacha majeraha ya muda mrefu. Siku ya kumbukizi iwe nafasi ya kusikiliza familia na jamii zilizoathirika, kutoa pole kitaifa, kujenga uaminifu na kuimarisha mazungumzo ya kitaifa. Maridhiano ya kweli yanapaswa kuwa jumuishi na kujengwa juu ya ukweli, haki, utu na dhamira ya kutorudia matukio hayo.



f) Kuimarisha Uwajibikaji wa Vyombo vya Usalama na Tahadhari za Mapema
Kumbukizi itoe nafasi ya kutathmini ulinzi wa raia, matumizi halali na yenye uwiano ya nguvu, mafunzo ya haki za binadamu na mifumo huru ya kuchunguza malalamiko. Pia ihamasishe utambuzi wa mapema wa viashiria vya migogoro, vitisho, lugha za chuki na matumizi mabaya ya mamlaka, ili hatua za kuzuia madhara zichukuliwe kwa wakati.

g) Kulinda Demokrasia, Utawala wa Sheria na Haki wakati wa Uchaguzi
Michakato ya uchaguzi inapaswa kuheshimu haki za kisiasa, uhai, uhuru wa kujieleza na haki ya kukusanyika kwa amani. Kumbukizi iwe jukwaa la kutafakari elimu ya uraia, uvumilivu wa maoni tofauti, usuluhishi wa migogoro kwa njia za kisheria na maboresho ya mifumo ya uchaguzi na usalama wa wananchi. Siku hii Itusaidie kutafakari namna bora tunaweza endesha shuhguli zetu za uchaguzi hapa nchini.

h) Kujifunza Kutokana na Uzoefu wa Kimataifa
Rwanda wana kumbukizi ya mauaji ya kimbari kuanzia 7 Aprili kukumbuka mauaji ya kimbari dhidi ya 1994; Afrika Kusini hutambua 21 Machi kama Siku ya Haki za Binadamu inayohusiana na mauaji ya Sharpeville ya 1960; na Umoja wa Mataifa hutambua 9 Desemba kwa kumbukizi na utu wa wahanga wa mauaji ya kimbari na kuzuia uhalifu huo. Mifano hii inaonesha nafasi ya kumbukizi katika kuenzi wahanga, kufundisha historia na kuzuia ukatili.

3. PENDEKEZO RASMI LA THRDC

Katika kujenga kumbukizi yenye maana, uponyaji wa kitaifa na maridhiano ya kweli, tunakumbushwa na mafundisho ya dini zote mbili kwamba haki, rehema, msamaha, amani na ulinzi wa uhai ni misingi muhimu ya jamii yenye mshikamano. Qur'an inatufundisha kuwa ***"Waumini ni ndugu; basi patanisheni kati ya ndugu zenu" (Qur'an 49:10),*** jambo linalosisitiza wajibu wa kujenga maridhiano na kurejesha mahusiano yaliyovunjika. Aidha, ***Qur'an 41:34*** inatukumbusha kujibu uovu kwa namna iliyo bora zaidi ili uhasama uweze kubadilishwa kuwa ukaribu. ***Qur'an 42:40*** inaunganisha haki na msamaha, huku ikitoa nafasi kwa maridhiano na kurekebisha madhara yaliyotokea. Vilevile, ***Qur'an 2:178–179*** inasisitiza thamani ya uhai, haki na uwajibikaji, na kutukumbusha kwamba kulinda maisha na kuzuia madhara ni msingi wa jamii yenye amani.



Kwa upande wa Biblia pia inaunganisha haki, amani na uponyaji. ***Wakolosai 3:13–15*** vinahimiza kuondoa uchungu, hasira na uadui na badala yake kujenga huruma, msamaha, upendo na amani. ***2 Wakorintho 5:18–19*** inaeleza maridhiano kama jukumu muhimu la kurejesha mahusiano yaliyovunjika, huku ***Mithali 15:1*** ikikumbusha kwamba jibu la upole linaweza kupunguza hasira na kuzuia migogoro kuongezeka. Kwa maana hiyo kutenga tarehe 29 kuwa siku ya kumbukizi ya 29 Ocober ni kujibu uovu kwa upole na kubadili uhasama kuwa mshikamano. ***"Those who cannot remember the past are condemned to repeat it. (Wasioweza kukumbuka historia wapo katika hatari ya kuridia historia)*** - George Santayana, 1905

Mafundisho haya yanaendana moja kwa moja msisitizo wetu kuwa na kumbukizi ya kitaifa haitalenga maombolezo pekee, bali pia kutafuta ukweli, kutenda haki, kuwaenzi wahanga, kuponya majeraha, kujenga upya uaminifu na kuhakikisha matukio kama hayo hayajirudii tena. Kwa msingi huo, kumbukizi inaweza kuwa jukwaa la kitaifa la kuunganisha jamii, kuimarisha mshikamano na kujenga utamaduni wa haki, amani na maridhiano.

a) Kumbukizi ya kwanza ifanyike 29 Oktoba 2026, kwa ushirikishwaji wa familia za wahanga, taasisi za umma, viongozi wa dini, asasi za kiraia na wananchi. Zifanyike kitaifa, kimkoa na kiwilaya.

b) Siku hiyo iwe ya maombolezo, tafakuri, elimu, ibada, haki, mshikamano na dhamira ya "Yasijirudie Tena", bila chuki au kulipiza kisasi.

c) Uwepo utaratibu wa kuhifadhi kumbukumbu zilizothibitishwa, kwa ridhaa na usalama wa wahusika. Hatimaye kuwepo na Makumbusho rasmi ya matukio haya kwa ajili ya vizazi vijavyo.

d) Hatua za uchunguzi, haki na maboresho ya taasisi ziende sambamba na kumbukizi.

e) Ibada, sala na dakika za ukimya kwa ajili ya kuwaenzi waliopoteza maisha.

f) Ushuhuda wa hiari wa familia za wahanga na majukwaa salama ya kusikiliza mahitaji yao.

g) Kongamano la kitaifa kuhusu ukweli, haki, maridhiano na hatua za kuzuia ukiukwaji wa haki.

h) Maonesho ya kumbukumbu na nyaraka za kihistoria zinazothibitishwa.

i) Elimu kwa vijana, shule na vyuo kuhusu uhai, haki za binadamu na amani.

j) Taarifa ya kila mwaka ya tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo na maboresho.

4.0 HITIMISHO

THRDC inaamini uongozi wenye maono huacha urithi si kwa kufuta kumbukumbu za nyakati ngumu, bali kwa kuzikabili kwa ujasiri, kuzitafakari kwa hekima, na kuzitumia kujenga taifa lenye umoja, haki na maridhiano ya kudumu. Kwa maana hiyo, THRDC inatoa wito kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulipokea na kulifanyia kazi pendekezo la kutambua tarehe 29 Oktoba kuwa Siku ya Kitaifa ya Kumbukizi ya Wahanga wa Matukio ya Oktoba 2025. Kumbukizi hii isiwe njia ya kufufua chuki au kuongeza migawanyiko, bali iwe nafasi ya kuenzi maisha, kutafuta ukweli, kutenda haki, kujenga maridhiano na kuchukua hatua zinazopimika kuhakikisha matukio kama hayo hayajirudii. ***António Guterres: "Remembering the past is crucial to safeguarding the future." "Kukumbuka yaliyopita ni muhimu katika kuulinda mustakabali."***

"TUNAWAKUMBUKA WAHANGA, TUNAJIFUNZA KUTOKANA NA HISTORIA, NA TUNACHUKUA HATUA KUHAKIKISHA YASIJIRUDIE TENA." (NEVER AGAIN)

Mratibu Wa Kitaifa -THRDC- 23/10/2026



Wakili Onesmo Olengurumwa



Mikocheni B, Eyasi Road, P.O.Box 105926,
Dar Es Salaam, Tanzania

+255 769 642208

info@thrdc.or.tz

www.thrdc.or.tz

Tufuatilie kwenye mitandao ya kijamii

Tanzania Human Rights
Defenders Coalition

@thrdcoalition

@thrdcoalition